

# BARAZA LA HABARI TANZANIA



S.L.P 10160, Dar es Salaam, Tanzania  
Simu: +255-22-2775728 / 2771947  
Simu ya mkononi: +255-784-314880  
Nukushi: +255-22-2700370  
Barua pepe: media@mct.or.tz  
Tovuti: <http://www.mct.or.tz>  
Zanzibar Office: P.O. Box 3490,  
Tel/Fax: +255-24-2239728,  
E-mail: mctz@mct.or.tz

P.O. Box 10160, Dar es Salaam, Tanzania  
Tel: +255-22-2775728 / 2771947  
Mob: +255-784-314880  
Fax: +255-22-2700370  
E-mail: media@mct.or.tz  
Website: <http://www.mct.or.tz>

Septemba 17, 2010

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

*Kamati ya Maadili ya Baraza la Habari Tanzania yatolea maamuzi mashauri mawili katika kikao chake cha Septemba 14, 2010*

Kamati ya Maadili ya Baraza la Habari Tanzania imebatilisha adhabu ya kufungiwa kufanya kazi kwa waandishi wawili wa Mkoa wa Pwani kwa mwaka mmoja na kuasa vyama vya wanahabaria kuzingatia, sheria, kanuni na taratibu katika maamuzi yao.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili, Jaji Mark Bomani alisema katika kusimamia weledi na maadili vyama vya waandishi wa habari visichukue hatua ambazo zitaathiri uhuru wa wanahabari kutenda kazi zao na kuwaumiza. Alisema Baraza la Habari Tanzania kwa muda mrefu limekuwa ikishirikiana na wadau wengine katika tasnia ya habari kuhakikisha kuwa wanahabari wanafanya kazi katika mazingira mazuri bila ya woga wa kudhuriwa au kuzuiliwa na itakuwa kinyume cha matarajio hayo kama kutakuwa na vyama vya wanahabari ambavyo vitachukua hatua za kuzuia wanahabari wasifanye majukumu yao kwa sababu yeyote ile.

Waandishi wawili wanaofanya kazi Mkoa wa Pwani, Grace Semfuko na Zainab Kihate walifungua malalamiko kwenye Baraza dhidi ya maamuzi ya Klabu ya Wanahabari wa Mkoa wa Pwani (CPRC) kuwafungia wasifanye kazi ya uandishi mkoani hapo kwa mwaka mmoja. CPRC waliambia Kamati kuwa walichukua hatua hiyo baada ya wanahabari hao kwenda kinyume cha maadili kwa kuitisha mkutano wa waandishi wa habari na kutoa taarifa ya kutangaza mgogoro dhidi ya Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo ambapo walimtuhumu kutokuwa na ushirikiano nao.

Pia CPRC ambayo iliwakilishwa na Mwenyekiti wake, Masau Bwire, ilisema kuwa walipata malalamiko kutoka kwa Mkuu huyo wa wilaya akiwatuhumu wanahabari hao kwa kumkashifu na kuandika habari nyeti. Semfuko na Kihate walikana madai hayo na kusema kuwa hata hiyo taarifa kwa vyombo vya habari ambayo ililetwa mbele ya Kamati hawaitambui na wala haina saina zao.


Waandishi hao waliambia Kamati kuwa CPRC waliandika barua kwa wakuu wa wilaya za Mkoa wa Pwani wakiwaeleza kuwa wamewafungia kwa mwaka waandishi hao kitendo ambacho kiliathiri utendaji kazi wao mkoani hapo kwani hawakuweza kupata ushirikiano wa viongozi wa mkoa huo. Semfuko anaandikia *Star TV* na *Radio Free Africa* wakati Kihate anaandikia gazeti la *Nipashe*.

Kamati ya Maadili pia imetoa anagalizo kwa wahariri kuwa waangalifu kuhusu habari zinazochapishwa kwa kuhakikisha kuwa habari hizo ni sahihi, zimezingatia pande zote na kutoa haki ya kujibu. Jaji Bomani alisema kuwa ukweli ndio nguzo kuu ya uandishi wa habari na juhuzi zote ni lazima zichukuliwe kuhakikisha kuwa habari zinazochapishwa ni za kweli. Jaji Bomani alisema hayo wakati akitoa maamuzi ya Kamati ya Maadili kuhusu shauri lililoletwa na Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) dhidi ya gazeti la *Umma Tanzania*.

Alisema kuwa vyombo vya habari ni taasisi zenye nguvu kwa hivyo ni muhimu kuhakikisha kuwa nguvu hizo zinatumiwa vizuri. Pia aliwataka wahariri kuzingatia na kusimamia maadili ya uandishi wa habari. ZECO walileta malalamiko yao kwenye Baraza kuhusiana na habari iliyochapishwa kwenye ukurasa wa kwanza wa gazeti la *Umma Tanzania* la Februari 11 - 18, 2010 yenye kichwa cha habari "Ufisadi waitafuna Zanzibar. Umeme sasa ni ndoto visiwani. Ni baada ya kununua kifaa bandia cha umeme."

Mwakilishi wa ZECO Abbas Juma Fakih aliambia Kamati kuwa habari hiyo iliyochapishwa kwenye gazeti haikuwa na ukweli wowote na kuwa iliharibu jina la shirika hilo mbele ya wananchi, serikali na wahisani wao. Jaji Bomani alisema kuwa maelezo ya Mhariri Mkuu wa gazeti hilo, Hamisi Kasabe, kuwa habari hiyo haikuihusu ZECO kwani hakuna mahali kwenye habari hiyo ambapo ZECO imetajwa haina mashiko kwani inafahamika dhahiri kuwa ZECO ndilo shirika pekee lenye kusambaza umeme Zanzibar na vilevile kusimamia mitambo na vifaa vyote vinavyohusika na kusambaza umeme visiwani.

Hivyo basi, Kamati iliona kuwa gazeti la *Umma Tanzania* liliandika habari potofu ambayo haikufanyiwa utafiti wa kina na kuwa habari hiyo ilidhuru ZECO, na hivyo kumwagiza Mhariri Mkuu aombe radhi kwenye toleo lifuatalo la gazeti lake. Pia Kamati iliagiza gazeti lilipe shirika hilo gharama zake za kusimamia shauri hilo kwenye Baraza.



k.n.y. Kajubi D. Mukajanga  
Katibu Mtendaji